Toleo la 12

Januari—Machi 2009

Banana Investments Limited

Mbiu ya Banana

YALIYOMO

1. BODI YA KAMPUNI YA BANANA YAZINDULIWA 2
2. 2
3. 3
4. 3
5. 4
6. ELIMU HAINA MWISHO 5
7. SERA YA UGAVI YA KAMPUNI YA BANANA HII HAPA…….... 6
8. UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU YA KAMPUNI YA BANANA WAANZA 6
9. WAKAZI WA OLOIRIEN WAPATIWA SEMINA YA UKIMWI 6
10. AJIRA MPYA KAMPUNI YA BANANA 7
11. MAANDALIZI YA TIMU YA MPIRA YA KLABU YA BANANA KWA LIGI YA WILAYA 8
12. WANACHAMA WA KLABU YA MICHEZO YA BANANA WASHIRIKI UTALII WA NDANI 8

KAMATI YA UHARIRI

Augustine S. Minja—Mwenyekiti

Beatha A. Massawe– Katibu

Patrick S. Mushi—Mjumbe

Philbert A. Muhindi – Mjumbe

Gerald E, Lyimo—Mjumbe

Banana Investments Limited

Makao Makuu: Oloirien Village, SLP 10123 ARUSHA, Simu 027 250 6475,

075 422 4440, 075 488 8470. Fax 027 250 1549. Email banana@bol.co.tz

……

Dar es Salaam Depot: Ubungo Kibangu, karibu na Kituo cha Poilisi cha

Ubungo Kibangu, SLP: 79407 Dar es Salaam, Simu: 022 277 4276, 075 670 7983.

……

Tanga Depot: Barabara ya 4, karibu na Stendi ya Mabasi ya TAWAKAL,

S.L.P. 5150 Tanga, Simu: 027 264 6134.



For more details, please visit our website on (http://www.banana.co.tz)

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.12, Januari—Machi 2009

SAFU YA MHARIRI

BODI YA KAMPUNI YA BANANA YAZINDULIWA

Kampuni inavyoendelea kukua kuna mabadiliko mbalimbali yanayoendana na ukuaji huo. Mnamo tarehe 29 Desemba 2008, kwa mara ya kwanza uongozi wa kampuni ulitambulishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Banana. Bodi hiyo iliteuliwa karibuni na ina wajumbe wanne.

Mwenyekiti wa Bodi ni Bwana Adolf R. Olomi na Makamu wake ni Bi. Alphoncina A. Olomi. Wajumbe wengine wa Bodi ni Dr. Donath R. Olomi na Bwana Charles S. Marunda.

Wajumbe wa Bodi walipata fursa ya kutembalea kiwanda na kisha wakafanya mkutano na viongozi wa kampuni. Baada ya utambulisho mfupi Mwenyekiti alizungumzia kuhusu sera na nyaraka mbalimbali zinazoongoza kampuni kiutendaji.

Imeandikwa na
Philbert A. Mhindi

WAJUMBE WA BODI YA KAMPUNI YA BANANA
Kutoka kushoto: Bi. Alphoncina A.Olomi, Bwana Adolf R. Olomi, Bwana Charles S. Marunda na Dr. Donath R. Olomi.

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.12, Januari—Machi 2009

USTAWI WA WAFANYAKAZI NA AFYA YA JAMII

ELIMU HAINA MWISHO

Mara nyingi utasikia watu wakisema kuwa elimu haina mwisho.Sote tunakubali kuwa huu ni ukweli usiopingika lakini ni vyema tujiulize: "Ni wangapi wanaotekeleza hili kwa vitendo? Je, hali katika sehemu zetu za kazi ikoje? Ni mashirika ama makampuni mangapi yanatekeleza wito huu kwa vitendo? " Hakika kama yapo ni machache sana.

Hii ndio sababu inayonifanya niipongeze Kampuni ya Banana kwa jitihada zake za kuendeleza wafanyazi wake kielimu. Kampuni hii licha ya kugharamia mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi wake, sasa imepig hatua nyingine muhimu kwa kuanzisha maktaba kwa ajili ya wafanyakazi wake.Maktaba hii ina vitabu vya fani mbalimbali kama biashara, uhasibu, uhandisi, computer, uongozi, sheria n.k. Pia yanapatikana magazeti ya kila siku na majarida ya taaluma mbalimbali.

Wakati wa mapumziko ya mchana maktaba huwa wazi na wafanyakazi hutumia muda huo kusoma magazeti ya kila siku na majarida mbalimbali. Pia wafanyakazi wanaruhusiwa kuazima vitabu kwa ajili ya kujisomea majumbani mwao.

Kuna baadhi ya makampuni yanayogharamia mafunzo kwa wafanyakazi wao lakini sina uhakika kama kuna ambayo yana maktaba kwa ajili ya wafanyakazi wao.

Ndio maana nasema kuwa Banana Investments Ltd inastahili kupongezwa kwa hilo.

Wakati tunaipongeza Kampuni ya Banana, kuna swali ambalo sisi wafanyakazi wa Kampuni ya Banana tunapaswa kujiuliza:"Je, ni wangapi miongoni mwetu tunatumia fursa hii adimu? "Jibu unalo wewe.

Imenipasa kuuliza swali hili kwa sababu sisi Watanzania, tofauti na wenzetu, hatuna tabia ya kujisomea. Wengi wetu tunasoma tu wakati wa kujiandaa kwa mitihani ama usaili. Tunapomaliza mitihani ndio mwisho wetu wa kusoma.Ukweli huu unajidhihirisha wazi ndani ya mabasi ya masafa marefu tunayosafiria.Mara nyingi mabasi haya hubeba zaidi ya abiria hamsini na husafiri kwa muda usiopungua saa nane.Ukichunguza abiria wote hawa ni kwa nadra utafanikiwa kupata 5% ya watu hawa wakisoma vitabu au magazeti. Badala yake utakuta abiria wengi wakisinzia au kupiga gumzo tu.Hii ndio hali halisi ya usomaji wetu sisi Watanzania.

Sipendi kuingia kwa undani kuhusu aina ya magazeti yanayosomwa zaidi lakini busara ya kawaida ni kuwa yale magazeti yanayosomwa kwa wingi ndiyo tunayogetegemea kutupatia matangazo mengi ya biashara, habari mpya na burudani mbalimbali. Tujiulize: "Ni kwa nini sisi hatujitumi kufanya hivyo?"

Sijapata bahati ya kwenda China lakini nilipata kusoma makala moja iliokuwa ikielezea jinsi Wachina wanavyopenda kujisomea. Ukiingia kwenye treni ama mabasi utakuta zaidi ya asilimia tisini na tano ya abiria wanasoma magazeti au vitabu. Hata waliokosa nafasi za kukaa utawaona wanasoma wakiwa wamesimama.Kupenda kwao kujisomea kumechangia kwa kiasi kikubwa kasi yao ya maendeleo tunayoishuhudia kwa sasa.

Hakika nchi haiwezi kuendelea kama raia wake hawana tabia ya kupenda kujisomea.Uongozi wa Kampuni ya Banana unalitambua hili na ndio hasa sababu ya kuanzisha maktaba kwa ajili ya wafanyakazi wake.

Sisi wafanyakazi tumweshapewa maji. Ni uamuzi wetu kuyanywa ama kuyaacha.

Nilimwuliza msimamizi wa maktaba ya Banana Investments Ltd, Bi Beatha Antony kama majirani zetu wanaotuzunguka wanaweza nao kupata fursa ya kutumia maktaba hii.

Alicheka na kusema kuwa angefurahi sana kama jambo hili lingewezekana na hapo hapo akanikumbusha kuwa lazima nijue kuwa Jiji la Roma halikujengwa siku moja. Polepole tutafika.

Watanzania tujirekebishe. Tusome.

Imeandikwa na
Gerald Lyimo

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.12, Januari—Machi 2009

USTAWI WA WAFANYAKAZI NA AFYA YA JAMII

SERA YA UGAVI YA KAMPUNI YA BANANA HII HAPA……...

Katika kipindi cha 2008 Kampuni ya Banana imeandaa sera .mbalimbali za uendeshaji kuendana na ukuaji wake. Sera inayosimamia ugavi ni mojawapo ya sera muhimu zilizopewa kipaumbele. Kampuni ya Banana iliandaa semina iliyoshirikisha wakuu wa idara na wafanyakazi wote wa idara ya ugavi. Semina hiyo ya siku moja Lilifanyika katika ukumbi wa City Link Hotel Desemba 12, 2008

Katika semina hiyo wawezeshaji walieleza taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika kutoa huduma za ugavi kwenye kampuni bila ya kukiuka sheria inayosimamia ugavi nchini Tanzania.Wanasemina walielezwa jinsi kila mfanyakazi wa Kampuni ya Banana anavyohusika na ugavi katika nafasi yake kazini.Ilisisitizwa kuwa kila mfanyakazi anatakiwa kufuata taratibu za ugavi na wafanyakazi wa idara hiyo wakaaswa kutoa huduma kila mara bila ya kukiuka maadili ya taaluma ya ugavi.

Waendeshaji wa semina walisifu taratibu za ugavi zinazofuatwa na Kampuni ya Banana na wakasisitiza kuwa lengo la semina lilikuwa ni kujiweka sawa na kuandika toleo la kwanza la sera ya ugavi kwa faida ya wafanyakazi na washika dau wengine. Sera hii itakuwa dira ya utendaji katika masuala yanayohusu ugavi na kila mtu anaweza kuirejea mara kwa mara badala ya kutoa huduma za ugavi bila ya mwelekeo unaokubalika.

Imeandikwa na
Philbert A. Mhindi

BAADHI YA WANASEMINA KWENYE UKUMBI WA CITY LINK HOTEL

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.12, Januari—Machi 2009

MICHEZO NA BURUDANI